

RUWASA inavyomaliza shida ya maji Songea

Na Albano Midel

WILAYA ya Songea, mkoani Ruvuma inatarajia kutumia zaidi ya Sh bilioni 5,799 kutekeleza miradi nane ya maji katika kipindi cha mwaka 2020/2021 katika halmashauri tatu zinazounda wilaya hiyo ambazo ni Manispaa ya Songea, Halmashauri ya Madaba na Halmashauri ya Songea.

Meneja Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijiini (Ruwsa) wilayani Songea, Mathias Charles, anasema hadi kufikia Januari mwaka huu Ruwsa wilayani Songea imopeka zaidi ya Sh milioni 877 sawa na asilimia 15.12 ya bajeti iliyopangwa.

"Hadi kufikia Januari 2021 wakazi wanaopata huduma ya maji wilaya ya Songea wanakadiria kuwa 132,362 sawa na asilimia 63.6 ya wakazi wote", anasema Charles.

Hata hivyo anabainisha kuwa hadi sasa mamlaka hiyo imetumia zaidi ya Sh bilioni tatu kutekeleza miradi tisa ya maji katika wilaya hiyo na kwamba Ruwsa inaendelea na kazi ya uboreshaji ya huduma ya upatikanaji ya maji kwa kujenga miradi mipywa.

Kulingana na Meneja huyu, Ruwsa inaendelea kukarabati miradi iliyokuwa imechakaa na kuboresha usimamizi wa miradi ya maji iliyokamilika ili iwe endelevu kwa kuunda na kusajili Jumuiya za Watumiaji Maji (CBWSOs) ambazo zitakuwa zinasimamia miradi hiyo na kuhakikisha inatoa huduma wakati wote.

Charles anasema katika kipindi cha mwaka 2019/2020 Ruwsa wilayani Songea ilipanga kuunda na kusajili jumuiya za watumiaji maji 17 ambapo hadi kufikia Juni 2020 jumuiya 10 zilikuwa zimeundwa na kusajiliwa.

Hata hivyo anasema kwa mwawa wa fedha 2020/2021 jumuiya za watumiaji 28 zilipangwa kuundwa na kusajiliwa ambapo hadi kufikia Januari 2021 jumuiya 11 zimeundwa.


Anaita miradi ya maji iliyopangwa kutekeleza

katika Halmashauri ya Madaba kupitia P4R kuwa ni Ndelenyuma, Lutukira na Mbangamawe, kupitia PBR4 mradi mmoja wa maji katika kijiji cha Igewisenga unatarajia kutekeleza.

Kwa mujibu wa Meneja huyu, katika Halmashauri ya Songea Vijiini kupitia P4R miradi ya maji inatarajia kutekeleza katika viji viine ya Lipaya, Lundusi na Maposeni.

Kupitia PBR4 mradi mmoja wa maji unatarajia kutekeleza katika kijiji cha Ndongosi na mradi mmoja unatarajia kutekeleza Ndilimalitembo, Manispaa ya Songea.

Anasema Ruwa-wilayani humo imepanga kukamilzoezi usajumuiya watumiaji kapo Juni 30 mwaka huu na



kwamba Ruwsa imejipanga kuendelea kutoa elimu juu ya utunzaji vyanzo ya maji na elimu kuhusu umuhimu wa ulipaji wa huduma ya maji ili kuifanya miradi iwe endelevu.

Akizungumzia Ruwsa inavyotekeliza miradi wa maji wa Sh bilioni 1.03 katika Halmashauri ya Madaba kwenye viji viine ya Mtepa, Kipingo, Lituta na Madaba,

Charles anasema miradi umekamilika kwa zaidi ya asilimia 90 na tayari wa-


wananchi.

Hata hivyo anasema ili kukamilisha tangi moja la Madaba Pachani zinasubiriwa pampu za kusukumia maji ambazo zitafungwa wakati wowote kuanzia sasa na kwamba mradi huo ni mkubwa umehusisha ujenzi wa matangi mawili na ulazaji wa mabomba kilometry 34.

"Wananchi wameanza kupata maji, tunatarajia maeneo mengine yaliyobakia hadi mwishoni mwa mwezi Januari hii wataanza kupata huduma ya maji, tunamshukuru Rais kwa kutupatia fedha zilizotekeliza mradi huu hivyo kuondoa kero ya maji kwa wananchi", anasema Charles.

Diwani wa Lituta katika Halmashauri ya Madaba, Olaph Pilli, anasema kabla ya kutekeleza mradi huu, Madaba ilikuwa na changamoto kubwa ya maji ambapo amesema mradi huu wa maji umekuwa mkombizo mukubwa katika kata yake.

"Hali ya maji katika Halmashauri yetu ya Madaba hasa katika Kata ya Lituta ilikuwa ni tete, wananchi



Diwani wa Kata ya Lituta Olaph Pilli akifungua maji ya bomba katika Shule ya Sekondari Madaba yaliyopanza kutoka Januari 18 na kumaliza kero ya maji katika sekondari hiyo.

walikuwa wanapata shida ya maji, lakini baada ya mradi huu sasa Madaba haitakuwa na shida tena ya maji, tuna maji ya kutosha", alisitiza diwani huyo.

Diwani Pilli anasitsa kuwa tayari maji yapo kwa wananchi wa Lituta na kwamba wanfunzi wa sekondari ya Madaba sasa wanafuraha kubwa baada ya kupata maji ya bomba hivyo kumaliza kero ya maji ya muda mrefu.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Jumuiya ya Watumiaji Maji viji vine ya Mtepa, Kipingo, Lituta na Madaba, Modestus Mgina, anaipongeza Ruwsa kwa kukamilisha ujenzi wa mradi huo na sasa wananchi wameanza kupata maji.

Anasema mradi huo utawanutaisha wananchi zaidi ya 19,000. Anasema hali ya maji kabla ya kutekeleza mradi huo ilikuwa ni mbaya kwani wananchi walikuwa wanapata maji ya mgawo kati ya siku tatu hadi tano.

"Maji yahikuwa yanapatikanwa kwa vurugu na ugomvi mukubwa, ilikuwa ni vita ya maji, lakini sasa sasa mradi



Mradi wa maji kijiji cha Lituta, Halmashauri ya Madaba uliogharimu zaidi ya Sh bilioni 1.03.